# Misri ya kale

## Misri ya kale na mto Nile

Eneo kubwa la Misri ya kale lilikuwa jangwa.

Bila ya kuwepo mto Nile isingewezekana binadamu kuishi. Mto Nile ni mto mrefu zaidi duniani na unapita nchi mbalimbali. Katika nchi ya Misri mto Nile upo kwa upana zaidi na unatiririka kuelekea bahari ya Medeterania.

Kama ilivyokuwa kwa mji wa kale wa Mesopotamia, mto Nile ni muhimu kwa shughuli za kilimo na kuishi. Nchini Misri mafuriko yanakujaga katika nyakati/muda maalumu kila mwaka. Kila mwaka kuanzia mwezi wa saba mpaka mwezi kumi ni muda wa mafuriko. Kwa kuwa watu wa Misri walijua ni lini mafuriko yanakujaga, walijiandaa kwa kuweka ukuta wa ziada kuzunguka miji na maeneo yaliyokuwa wazi/mashamba, na kumwaga maji yaliyokuwemo kwenye mabwawa makubwa ya maji. Mafuriko Misri hayakuwa makubwa sana kama ilivyokuwa kwenye mji wa Mesopotamia.

Wakazi wengi wa Misri walikuwa wakulima. Walilima chakula, walikuwa na wanyama wa kufuga nyumbani, waliwinda na kuvua samaki. Baadhi yao walikuwa wakifanya kazi za mikono, kama mafundi wa kujenga kwa matofali, kuoka/kupika, wajenzi wa boti/mitumbwi na watengenezaji wa vitu vya chuma/wahunzi.

Katika maeneo yaliyokuwa wazi/mashamba wakulima walilima kitani(aina ya mmea) ambapo wanawake waliitumia kusuka/kutengezea vitambaa. Katika maeneo yaliyokuwa karibu na kingo za mto familia zilikuwa zinakusanya aina fulani maalumu ya mmea uitwao mafunjo/**papyrus**. Kwa kutumia mmea huo wa mafunjo waliweza kutengeneza kati ya mambo mengine viatu, boti na karatasi. Neno karatasi linatokana na mmea huo.

Wamisri walitengeneza mfumo wa kuandika/uandishi unaoitwa **hieroglyfer**. Wakati watu wa Mesopotamia waliandika kwenye meza zilizotengenezwa kwa udongo, Wamisri waliandika kwenye mafunjo/**papyrus**.



Tekst og bilder hentet fra Zmekk.no i samarbeid med NAFO – Nasjonalt senter for flerkulturell opplæring




*Kunstverk som illustrerer egyptiske båtbyggere og illustrasjon av hieroglyfer*

## Farao

Nchini Misri mfalme alikuwa mtu mwenye nguvu. Alikuwa na nyumba nzuri kubwa na kazi yake kubwa ilikuwa kuangalia kila mtu aliishi vizuri. Wamisri walikuwa wakiamini mfalme ni mtoto wa Mungu kwa hiyo hawakuthubutu kusema jina lake. Walimuita Farao jina lililokuwa linamaanisha “nyumba kubwa”. Ufarao ulirithishwa toka kwa baba hadi watoto wa kiume. Watu waliokuwa wanaishi/wakazi wa Misri walitakiwa kulipa kodi kwa farao. Hawakulipa kodi kwa pesa, kama tunavyolipa sasa, bali farao alilipwa sehemu ya vitu wanavyolima na kutengeneza katika nchi kama kodi. Farao alitengeneza mabwawa makubwa ya maji kwa ajili ya kuzuia mafuriko, mifereji ya kumwagilia na mahekalu. Watu ilibidi wasaidie kwenye hizo shughuli.

## Piramidi

Misri inajulikana duniani kwa kuwa na mapiramidi makubwa sana, ambapo ilikuwa sehemu ya kuzika baadhi ya wafalme wa nchi yao. Wamisri waliamini juu ya maisha baada ya kifo, hivyo ilikuwa muhimu wafalme wazikwe vizuri. Walizikwa pamoja na dhahabu, chakula, nguo na silaha ambazo zingetumika katika maisha yao baada ya kifo. Ili kuhifadhi miili ya watu waliokufa waliifunga miili kwa bandeji na kutengeneza maiti **mumier.**

Kwanza mtu aliyekufa alioshwa kwa njia maalumu, kisha ubongo na utumbo vilitolewa na kuwekwa kwenye mtungi tofauti na mwili unaozikwa. Moyo ulizikwa na Mwili wa farao. Mwili ulipakwa na kulainishwa kwa mafuta ya kunukia vizuri/marashi/manukato. Baada ya hapo mwili wote ulifungwa kwa kuzungushiwa bandeji. Mwisho walitengeneza mwili wa marehemu kama **mumien** ambapo uliwekwa kwenye jeneza maalumu na picha ya aliyekufa iliwekwa nje ya jeneza.



Tekst og bilder hentet fra Zmekk.no i samarbeid med NAFO – Nasjonalt senter for flerkulturell opplæring



*illustrasjoner som viser faraoer, Keopspyramiden og en mumie*

Farao wengi na watu waliokuwa matajiri, walizikwa kwenye mapiramidi yao pekee. Karibuni kulijengwa mapiramidi 50. Piramidi kubwa linaitwa piramidi kuu la Giza (**Keopspyramiden**) na inaitwa jina hilo la mfalme aliyezikwa hapo; mfalme **Keops** (alitawala kuanzia karibuni mwaka 2589 mpaka 2566 Kabla ya Kristo). Piramidi hili lipo kwenye jangwa katika mji uitwao Giza, eneo lilopo nje kidogo ya mji mkuu wa sasa wa Misri,  Cairo. Katika bonde la wafalme lilopo karibu na mji wa **Luxor** , makaburi ya kifalme na maiti (**mumier**) zimepatikana.



Tekst og bilder hentet fra Zmekk.no i samarbeid med NAFO – Nasjonalt senter for flerkulturell opplæring

## Je wajua?

- 96% ya sehemu ya nchi ya Misri ni jangwa.
- Mto Nile una urefu wa kilomita 6500.
- Piramidi za Misri ni moja kati ya maajabu saba ya dunia( Unaweza kutafuta maajabu mengine sita  ya dunia ni yapi)
- Piramidi kuu ya Giza (**Keopspyramiden)** ina urefu wa mita 137, na imejengwa kwa matofali ya mawe yapatayo milioni 2 ½.
- Ncha (sehemu iliyopo juu) ya piramidi ilitengenezwa kwa dhahabu.
- Piramidi nyingine zinapatikana Mexico na Peru.
- Vitu vya thamani/hazina nyingi vimeibiwa na wezi kwa miaka mingi.




Zoezi
Angalia vizuri alfabeti zilizopo hapo juu na andika neno unalopata kwa lugha ya Kinorway.


________________________________


_______________________________________


____________________________


_________________



Tekst og bilder hentet fra Zmekk.no i samarbeid med NAFO – Nasjonalt senter for flerkulturell opplæring